

JAMHURI YA MUUNGANOWA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA
MASHARIKI

Simu: +255-26-2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208
Barua pepe: nje@nje.go.tz
Tovuti: www.foreign.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtumba,
S.L.P 2933,
40466 DODOMA

FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO KWA WATANZANIA

Dodoma 18 Februari 2022

Wizara imepokea fursa za ufadhili wa masomo ya muda mfupi na muda mrefu katika kada mbalimbali kutoka Chuo kikuu cha Urafiki katika Shirikisho la Urusi (The Peoples Friendship University of Russia -RUDN) kwa mwaka wa masomo wa 2022-2023 na Jamhuri ya Mauritius kupitia programu yake ya *Ufadhili wa Masomo kwa Nchi za Afrika 2022*(AFRICA SCHOLARSHIP SCHEME 2022).

Fursa za masomo zilizotolewazinahusisha mafunzo ya muda mfupi, Shahada ya Kwanza, Mafunzo katika Fani Maalum (Specialists), Shahada ya Uzamili (Master's Program), na Shahada ya Uzamivu (PhD).

Taarifa zaidi kuhusu fursa mbalimbali za mafunzo haya zinapatikana kupitia viunga vya mtandao/Tovuti kama ifuatavyo: -

<https://www.rudn.ru/admissions/admission-for-foreign-citizens-2021/>

<https://education.govmu.org/Pages/Mauritius-Africa-Scholarships-2020.aspx>and<http://highereducationmauritius.com>

Aidha, waombaji fursa za ufadhili za Chuo Kikuu cha Urafiki katika Shirikisho la Urusi wanahimizwa kujisajili kwa njia ya mtandao kupitia Tovuti ifuatayo: <https://admission-2021.rudn.ru> .


Sheiba Bulu

Kaimu Mkurugenzi, Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali